

Je, Gel ni salama na kinga dhabiti dhidi ya HIV?

Gel ni salama kwa wanawake na wanaume. Haina madhara makubwa.

Gel inaweza kupunguza hatari ya mwanamke kupata Virusi vya HIV, hata hivyo si kwa ufanisi ya asilimia moja (100%). Gel itapunguza uwezekano wa mwanamke kupata virusi vya ukimwi kwa asilimia arobaini (40%) katika matumizi ya kawaida. Gel inapotumiwa kwa njia sahihi wakati wote mwanamke anapofanya ngono basi kiwango cha kinga dhidi ya virusi vya HIV inakuwa juu.

Ikiwa wanandoa tayari wanatumia kondomu, basi wasiache kuvitumia. Wanaweza kutumia Gel pamoja na kondomu ilikupata kinga ya ziada dhidi ya virusi vya HIV na Ukimwi.

Kama matumizi ya kondomu haiwezekani, basi Gel inaweza kutumika peke yake. Hata ingawaje haiwezi kukupatia kinga kamili fu dhidi ya virusi vya HIV, ni bora kuliko kukosa kinga kabisa.

Gel inakinga wanawake wasio na virusi vya HIV tu. Haiwezi kutibu HIV na ukimwi na haiwezi kuzuia wanaume kuambukizwa virusi vya HIV.

Gel haizuii kupata mimba. Wanawake wanapaswa kutumia kondomu au namna nyingine za kupanga uzazi iwapo hawataki kupata mimba.

Je, mwanamke anawezaje kupata Gel?

Hatua ya kwanza ni kutembelea kituo cha afya ambacho kinapeana Gel. Vituo vingi vinavyotoa ushauri nasaha na kupima HIV (HTC) na vile vinavyopeana huduma za mpango wa uzazi pia hupeana Gel. Wanawake wanaweza kwenda pekee yao au pamoja na wapenzi na waume wao.

Daktari au muuguzi hutoa ushauri na kusaidia mwanamke kuamua iwapo Gel inamfaa. Iwapo mwanamke angependa kujaribu kutumia Gel, ni lazima apimwe hali yake ya HIV. Kama atapatikana kuwa hana HIV, basi atapewa Gel kwenye kituo cha afya hicho ambapo alipata ushauri.

Wanawake wanapaswa kupimwa virusi vya HIV baada ya kila miezi 3 ili waweze kupata Gel zaidi.



Kwa maelezo zaidi:

Tembelea kituo cha afya kilicho karibu nawe
Tembelea tuvuti www.nagel.co.ke
Piga simu: 0800 000 000

@nagel /nagel



**Njia mpya ya
Kuzuia HIV
kwa wanawake**

Microbicide Gel



Je Gel ya Microbicide ni nini?

Wanawake wanaweza kuambukizwa HIV kwa kufanya ngono na mtu aliyeambukizwa bila kutumia kinga.

Microbicides ni aina ya Gel mpya kinachosaidia kizua virusi vya HIV. Zinaweza kusaidia kukinga wanawake dhidi ya virusi vya HIV kutokana na kufanya ngono bila ya kutumia kinga. Pia zinaweza kuzuia ugonjwa wa zinaa wa kawaida wa malengelenge (Herpes Zoster).

Microbicides huja kwa njia ya Gel ambayo huingizwa kwenye uke kabla na baada ya kufanya ngono. Gel itakupa kinga ya ziada iwapo kondomu haitatumika kwa njia sahihi. Pia inatoa kiasi cha kinga iwapo itatumika pekee.

Gel hiyo huongeza ulainishi kwenye uke. Wanawake na wanaume wengi wanatambua kwamba ulainishi huu inaongeza hamu na burudisho wanaposhiriki ngono. Gel huwezesha mwanamke kudhibiti nyakati na inamwezesha kuchukua usimamizi ya kinga yake mwenywewe.

Gel inaweza kutumika hata bila mume au mpenzi wake kujua. Hata hivyo wanawake wametambua kuwa ni rahisi kutumia Gel wakati wanapoungwa mkono na wanaume au wapenzi wao.

Nani anaweza kutumia Gel?

Gel inaweza kutumiwa na mwanamke yejote ambaye hana virusi vya HIV na anayeshiriki ngono. Inaweza kutumiwa na wanawake walio na wapenzi wasiowaamini, wanawake walio na wapenzi wa kiume na wanawake walio kwenye ndoa.

Jinsi ya kuingiza Gel kwenye uke



Gel itasaidia kuwakinga wanawake wasiojua hali ya HIV ya wapenzi wao au wenzao wa ndoa. Pia inaweza kuwalinda wanawake walio na wapenzi walio na virusi vya HIV.



Gel hutumiwa mara ngapi?

Gel ya kwanza inaweza kutiwa kwenye uke angalau dakika 15 kabla ya kushiriki ngono lakini sio zaidi ya masaa 12 kabla ya kushiriki ngono. Gel ya pili yafaa kutiwa kwenye uke mara tu baada ya kufanya ngono mara ya kwanza lakini haifai kuitisha masaa kumi na mbili baada ya ngono.

Haijalishi ni mara ngapi mwanamke anashiriki ngono, cha muhimu ni kuwa hafai kutia Gel zaidi ya mara mbili kwa muda wa masaa ishirini na nne. Kwa wanawake wengine, kutumia gel moja kila baada ya masaa kumi na mawili ndio njia mwafaka wa kupata kinga kwa siku ambazo atashiriki ngono.